Lugha ya Yohana ya Ishara

Sura ya 7

Somo la Kusikiza: Agano Jipya #25

Shabaha: Kuleta ufahamisho wa Injili ya Yohana na kuelewa mada na makusudi yake. muhimu.

Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake.

- Yohana 20:30-31

Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale walioamini jina lake; waliozaliwa si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli.

- Yohana 1:12-14

Injili ya Yohana ni Injili inayopendwa na mamilioni ya watu kwa sababu ya vile Mungu ameitumia kuwaleta kwa imani katika Yesu na kuwaonyesha Yeye ni nani Hasa. Ni ya kipekee katika njia nyingi; makusudi yake, mtindo wake wa uandishi, na yaliyomo na tofauti na yale ya Injili zingine. Mwamndishi – mwanafunzi aliyependwa sana aitwaye Yohana – alitumia lugha ya ishara na umbo, akitupa picha za Yesu zisizopatikana katika Injili zingine.

Ili kuelewa Injili ya Yohana, tunahitaji kutambuwa kuwa ingawa iliandikwa kutia nguvu na kuelimisha waumini, pia ilielekezwa haswa kwa wale wasioamini ili kuwaleta kwa imani. Yohana anatoa hoja ya kithiolojia kuhusu Yesu na anajibu maswali ya msingi kuhusu Yesu ni nani, na kwa nini alikuja. Yohana anaandikisha ishara nyingi au miujiza inayotia moyo na kutia imani nguvu na kuthibitisha kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu. Pia anatoa picha kadhaa za kupendeza za Yesu. Mtu anaweza kusoma Injili ya Yohana kwa juu juu na ajifunze mengi kuhusu Yesu, lakini Injili hii pia imeandikwa kwa kiwango cha undani ambacho mtu anaweza kuchunguza kwa maisha yake yote na awe bado hajapata yote.

Ona kuwa tunapojifunza Injili ya Yohana, anajibu maswali matatu: Yesu ni nani; Imani ni nini; na maisha ni nini? Unaposoma, tafuta majibu ya Yohana kwa maswali haya katika kila sura.

1. Ukweli au **uongo**? Injili ya Yohana inafanana kwa ukaribu sana na Injili zingine tatu na inajumuisha nyingi ya hadithi zinazofanana.

2. **Ukweli** au uongo? Kuongezea kwa Injili, Yohana pia aliandika Ufunuo wa Yohana na nyaraka zingine tatu za Agano Jipya.

3. **Ukweli** au uongo? Injili ya Yohana iliandikwa nyuma sana kuliko Injili zingine tatu.

4. Ukweli au **uongo**? Yohana aliandika Injili yake kwa waumini pekee na si kwa wasio amini.

Ikiwa hujaambiwa lingine la kufanya, basi, chagua jibu moja tu kwa kila swali lifuatalo.

5. Kwa nini Yohana alijumuisha "ishara" nyingi au hadithi za miujiza katika injili yake?

a. Kuthibitisha kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu, na kutia watu moyo kumwamini

b. Kufanya hadithi yake iwe ya kufurahisha

c. Kuonyesha kuwa waumini wa kweli kila mara watapata miujiza wakiwa na imani ya kutosha

d. Kuwafanya watu wasome injili yake kuliko injili zingine

6. Ni kwa njia gani injili ya Yohana inakuwa ya kipekee? *(Chagua yote yanayolingana)*

a. Iko na hoja taratibu

b. Imeandikwa kwa waumini na wasioamini

c. Inapeana maelezo mengi kuhusu kuzaliwa kwa Yesu na siku zake za utotoni

d. Imeandikwa kwa viwango viwili – kiwango rahisi kuelewa cha juu, na kiwango cha kina cha ujumbe mkuu.

e. Kinalenga kule kuwatokea wanafunzi kwa Yesu na kanisa la kwanza baada ya kufufuka kwake.

f. Mengi ya yaliyomo hayapatikani katika injili zingine.

7. Ni maswali gani makuu ambayo injili ya Yohana inatafuta kujibu? *(Chagua yote yanayolingana)*

a. Yesu alitimiza vipi unabii?
b. Yesu ni nani?
c. Yesu atarudi tena lini?
d. Kanisa la kwanza lilikuwaje?
e. Imani ni nini?
f. Maisha ni nini?

8. Ni gani kati ya picha za Yesu zifuatazo inayopatikana kwa Injili ya Yohana? *(Chagua yote yanayolingana)*

a. Maji ya uzima
b. Hakimu mkali
c. Mchungaji mwema
d.Kichaka kinacho ungua
e. Nuru ya ulimwengu
f. Mkate wa uzima
g. Ufufuo na uzima
h. Mzabibu
i. Mwana kondoo wa Mungu
j. Ngome kuu
k. Mtumishi
l. Kuhani mkuu
m. Chembe ya ngano

9. Yohana anamwita Yesu nani katika sura yake ya kwanza?

a. Mtu anayewaza kwa upeo wa juu
b. Neno la Mungu katika mwili
c. Mwalimu wa a jabu
d. Kiongozi wa ajabu wa kiroho

10. Sura ya kwanza pia inatwambia mambo gani mengine kuhusu wakati Yesu alikuja? *(Chagua yote yanayotumika)*

a. Wayahudi walimkataa Yesu
b. Yesu alitoa mamlaka kwa yeyote kumpokea
c. Wote wanaompokea Yesu watapona
d. Wote wanaoamini na kumpokea Yesu wanazaliwa mara ya pili

Wengi wa Wayahudi walimwitikia vipi Yesu? Yesu anataka wewe umwitikie vipi? Ni hatua gani ya imani unayoweza kujukuwa sasa hivi ili kumsongea Yesu na kuthibitisha tumaini ndani yake?

_____

_____

_____

Mshukuru Mungu kwa kutupatia kitabu hiki kinachotwambia kila tunachohitaji ili kumwamini Yesu, Mungu mwenyewe aliyefanyika mwili, na kuwa kupitia kumtumainia yeye tunao uzima wa milele. Muulize akuonyeshe kinachomaanisha na uzima tele na kukuongoza ndani ya imani ya kina zaidi unapojifunza Injili ya Yohana.

KUZAMA ZAIDI

1. Kulingana na aya mbili za mwisho za sura ya 20, kwa nini Yohana alishiriki nasi ishara nyingi sana? _____
_____
_____

2. Ni katika njia gani injili ya Yohana imeelekezwa kwa wasioamini? _____
_____
_____
_____

3. "Ishara" ni nini na aya ya mwisho ya injili ya Yohana inatwambia nini kuhusu hesabu ya ishara ambazo Yesu alitupea? _____
_____
_____

4. Kulingana na aya zake za kwanza 18, Yohana anatufanya tujue nini kwa udhahiri kuwa ni kile anaenda kutuambia katika Injili yake? _____
_____
_____
_____

5. Yohana anamaanisha nini anapotwambia kuwa hapo mwanza kulikuweko Neno, Naye Neno alikuwa Mungu, Neno aliumba kila kitu, Naye neno akafanyika mwili na akakaa kati yetu ili tuuone utukufu wake? _____
_____
_____

6. Yohana anamaanisha nini anapotwambia kuwa wale waliompokea hata wale waliomwamini, walizaliwa na Mungu? _____
_____
_____
_____

7. Wakati Yohana anaandika kuhusu wale "waliompokea" katika njia sawa, Je anamaanisha kuwa wakati Yesu alikuwa hapa katika mwili watu waliinamisha vichwa vyao na kumuuliza aingie mioyoni mwao? Elezea. _____
_____
_____